# Tanzania Ifikapo 2025

## Je, Watanzania wana matarajio gani ya maisha yao ya baadae?





## 1. Utangulizi

Mabadiliko nchini Tanzania ni yana mbili, yale yanayotokea pole pole na yale ya kasi. Wakati kaya nyingi za vijijini zinaripoti kuishi bila umeme, bila usafiri wa uhakika au kuwa na gari na bila nyumba bora, idadi ya watu katika jiji la Dar es Salaam imeongezeka karibu mara mbili katika kipindi cha miaka kumi kati ya mwaka 2002 na 2012. Idadi ya watu imeongezeka kutoka watu milioni 2.5 mwaka 2002 hadi watu milioni 4.4. Pato la Taifa lilikuwa dola za Kimarekani 316 mwaka 2001 na limengozeka zaidi ya mara mbili hadi dola za Kimarekani 652 kwa mwaka 2012[1]. Aidha miaka kumi iliyopita, watanzania wachache tu walikuwa wanamiliki simu za mkononi. Leo, mmoja kati ya Watanzania wawili ana angalau simu moja, na kaya nane kati ya kumi zinamiliki angalau simu moja ya mkononi[2].

Hivyo, mambo yamekuwa yakibadilika kwa kasi na kwa kiwango kikubwa: idadi ya watu wanaoishi mijini imeongezeka kwa kasi, wastani wa Pato la Taifa limeongezeka, na gesi asilia imekuwa suala muhimu la kitaifa kufuatia kugundulika katika sehemu za ukanda wa pwani. Je, sura na hali ya nchi yetu miaka kumi ijayo itakuwaje? Na je, wananchi wa kawaida wanaamini nini kitatokea kati ya sasa na mwaka 2025? Nini ni tafakari yao?

*Sauti za Wananchi* ya Twaweza ni utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu za mkononi (http://www.twaweza.org/sauti). Katika awamu ya 23 ya upigaji simu, utafiti huu ulifanyika kati ya tarehe 13 na 22 Agosti 2014 kwa ushirikiano na *Society for International Development (SID)*, na ulijumuisha wahojiwa 1,408 ili kupata maoni yao juu ya mustakabali wa Tanzania. Muhtasari huu unatoa maelezo ya jumla kutokana na majibu yao.

[1] NBS, Wizaya ya Fedha (2013), "Tanzania kati  a Tarakimu 2012". (http://  ww.nbs.go.tz/nbs/takwimu/references/Tanzania_in_figu es2012.pdf).

[2] Shirika la Maendeleo Kimataifa 2012, "Ripoti ya hali ya Afrika Mashariki 2012"; na Sauti za Wananchi, Muhtasari Na.1, Februari 2013 (http://www.twaweza.org/go/sauti-za-wananchi-swahili).

SID
Society for International Development

Muhtasari huu umeandikwa na Angela Ambroz, Aidan Eyakuze, Elvis Mushi na Youdi Schipper na kutolewa na Twaweza, iliyoko Hivos Tanzania, kwa kushirikiana na Society for International Development (SID) Tanzania. Imetolewa Desemba 2014

S.L. B 38342, Dar es Salaam, Tanzania. Simu: +255 22 266 4301
e: uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Matokeo muhimu ni:


- Mwananchi mmoja kati   a wawili anatarajia kwamba maisha yake yatakuwa bora zaidi kati  a siku zijazo, na idadi kubwa zaidi  wanajiona kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kustawisha maisha yao ya baadaye.
- Wananchi wawili kati   a watatu wanaamini kuwa nchi yetu itakuwa "mahali pazuri pa kuishi" ifi  apo mwaka 2025.
- Wananchi tisa   ati   a kumi wanaona kwamba maamuzi makubwa ya kitaifa yatakuwa chini ya udhibiti    a nchi yenyewe.
- Wananchi saba kati   a kumi wanaamini kwamba Tanzania itakuwa nchi ya kipato cha kati i    apo mwaka 2025, lakini wananchi wanne tu kati   a kumi wanaamini kuwa Tanzania itafuzu  kucheza mashindano ya Kombe la Dunia.
- Wananchi wameonesha kuwa  vipaumbele muhimu kwa maisha ya baadaye ni kuongeza ubora wa utoaji wa huduma za kijamii, ukuaji wa uchumi na umoja wa kitaifa.

# 2. Mambo sita kuhusu matarajio ya wananchi ifikapo 2025

## Jambo la 1: Mwananchi mmoja kati   a wawili anatarajia kwamba maisha yake yatakuwa bora zaidi siku zijazo

Walipoulizwa kufikiria juu ya maisha yao ifikapo 2025, Mtanzania mmoja kati ya wawili aliripoti kuwa anaamini kwamba maisha yake yatakuwa bora zaidi (Kielelezo cha 1). Hata hivyo, idadi kubwa kidogo; yaani mwananchi mmoja kati ya watano (18%) aliaamini kuwa maisha yake yatakuwa mabaya zaidi ifikapo 2015 (Kielelezo cha 1). Majibu ya swali hili hayakutofautiana sana kati ya mhojiwa mwanaume au mwanamke, tajiri au maskini, au hata kulingana na kiwango chake cha elimu, pamoja na kama anaishi maeneo ya vijijini ama mijini (takwimu hazijaoneshwa)[3].  Kwa ujumla, kila mtu aliyehojiwa aliwekwa kwenye kundi la kati ya wenye matumaini au wasio na matumaini juu ya hali zao za maisha katika siku zijazo.

**Kielelezo cha 1: Ifi  apo 2025, maisha yako yatakuwa…?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 23 (Agosti 2014)

[3] Takwimu na machapisho yote ya Sauti za Wananchi vinaweza kupakuliwa http://  ww.twaweza.org/go/sauti- a-wananchi-swahili.

Ili kulinganisha matokeo haya na wastani wa kikanda na kimataifa, tumetumia takwimu kutoka mradi wa Utafiti a Mitazamo Duniani[4] wa kituo cha utafiti ch *Pew Center* wa mwaka 2014. Utafiti huu unaofanyika duniani kote uliuliza kama watu wanaamini watoto wao watakuwa na hali ya maisha nzuri zaidi au mbaya zaidi kuliko wazazi wao. Kwa ujumla, karibu mhojiwa mmoja kati ya wawili kutoka nchi za Afrika aliamini kwamba mtoto wake atakuwa na hali bora zaidi ya kifedha (Kielelezo cha 2). Hii ni tofauti kabisa na nchi zilizoendelea – barani Ulaya na Marekani - ambako watu wengi zaidi waliamini kuwa watoto wao watakuwa na hali mbaya zaidi ya kifedha (Kielelezo cha 2).

**Kielelezo cha 2: Watoto nchini kwetu watakuwa na hali bora zaidi au mbaya zaidi kuliko wazazi wao kati a miaka ijayo?**




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa Mitazamo Duniani wa *Pew Research Center* 2014

## Jambo la 2: Mwananchi mmoja kati a wawili anajiona kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kustawisha maisha yake ya baadaye

Walipoulizwa kuhusu nani atakuwa na ushawishi mkubwa juu ya ustawi wa maisha yao ya baadaye, mwananchi mmoja kati a wawili amesema ni wao wenyewe (Kielelezo cha 3). Hii imeendana na mawazo kuhusu utayari wa wananchi kushiriki kati a maisha yao wenyewe ilivyoripoti a na Sauti a Wananchi kati a muhtasari wa Wananchi na uchu wa mabadiliko. Kati a muhtasari huo; wananchi tisa ati a kumi walikubaliana na maelezo yafuatayo: “Ni rahisi kwangu kujikita kwenye malengo yangu na kutimi a matarajio yangu”, na, “Kama niko kwenye matati o, siku zote naweza kufikiria ufumbuzi na u atuzi mwenyewe” (takwimu hazikuoneshwa)[5].


Hata hivyo, “vishawishi” vikubwa vitatu vinatofautiana ati a kaya za mijini na vijijini. Wahojiwa wa mijini wanaona vishawishi vikubwa zaidi kwenye maisha yao kuwa ni: wao wenyewe (57%), familia zao (20%), na marafiki au enzao (19%) (Kielelezo cha 3). Hii ilikuwa tofauti sana k a wahojiwa wa vijijini ambao walisema chenye ushawishi mkubwa ni wao wenyewe (56%), ni serikali (20%), na familia zao (19%) (Kielelezo cha 3).

---

[4] Pew Research Center, Oktoba 2014. “nchi zenye uchumi unaibuka na unaoendelea zina matumaini zaidi na hali ya maisha yao siku zijazo”. http:// ww.pewglobal.org/2014/10/09/emerging-and-developing-economies-much-more-optimi tic-than-rich countries-about-the-future/

[5] “Wananchi wanaleta mabadiliko.” Septemba 2014. http://t aweza.org/uploads/files/Ci enAgency-EN-FINAL.pdf

**Kielelezo cha 3: Nani mwenye ushawishi mkubwa kwenye ustawi wa maisha yako?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 23 (Agosti 2014)

## Jambo la 3: Wananchi zaidi ya nusu wana matumaini kuhusu Tanzania

Tukiachana na masuala binafsi, Watanzania wana matumaini makubwa pia kwenye masuala ya kisiasa. Wananchi wawili kati   a watatu wanaamini kuwa nchi itakuwa “mahali pazuri pa kuishi” ifi  apo 2025, idadi inatofautiana kido  o tu kwa kulinganisha kati   a  wananchi maskini zaidi na matajiri; (maskini wana matumaini zaidi, 68%) na matajiri (64%) (Kielelezo cha 4). Hata hivyo, tofauti hizi hazina maana   ubwa kitakwimu. Tukiangalia takwimu hizi kwa mtazamo tofauti, tu aona kuwa mtu mmoja kati   a wanne kwenye kundi la wananchi matajiri anaamini kuwa nchi itakuwa “mahali pabaya pa kuishi” ifi  apo mwaka 2025.

**Kielelezo cha 4: Ifi  apo 2025, unafikiri   anzania itakuwaje...?**





*Majibu ya “Sijui” na wasiojibu yameondolewa.*

**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 23 (Agosti 2014)

## Jambo la 4: Wananchi tisa ati a kumi wanaamini kwamba maamuzi muhimu yatabaki chini ya udhibiti a kitaifa

Kama wanavyoamini kuwa hatma ya ustawi wa maisha yao ya baadaye iko mikononi mwao wenyewe (Jambo la 2), wananchi tisa kati ya kumi wanaamini pia kuwa mustakabali wa Tanzania uko mikononi mwa Watanzania wenyewe: Ama kupitia viongozi wa nchi, au wananchi wenyewe (Kielelezo cha 5). Wawekezaji wa kigeni na wafadhili wanaonekana kuwa na udhibiti kidogo sana kwenye masuala muhimu - kwa mfano, hakuna mtu hata mmoja aliyetaja Umoja wa Mataifa kuwa na udhibiti, (Kielelezo cha 5). Kutokana na nchi kutegemea misaada ya wafadhili katika kuchangia baje [6] na kutokanan na uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja kuchangia mapato kutokana na utalii na mauzo ya nje ya madini, haya ni matokeo ya kuvutia. Watanzania wasomi wanaonekana kutokuwa na umuhimu mkubwa kwa 0.1% au mtu 1 kati ya watu 1000 waliohojiwa (Kielelezo cha 5).

**Kielelezo cha 5: Ifi apo 2025, unafikiri nani takuwa na udhibiti m ubwa juu ya maamuzi muhimu nchini Tanzania?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 23 (Agosti 2014)

## Jambo la 5: Wananchi wanasema, utoaji huduma, ukuaji wa uchumi na umoja wa kitaifa ni vipaumbele kwa siku zijazo

Wakati wananchi wanajibu swali lililouliza ni mambo gani wanafikiri yawe vipaumbele muhimu vya nchi kwa siku zijazo, mambo muhimu zaidi kwao yalikuwa ubora wa huduma za umma kama elimu na afya (28%)(Kielelezo cha 6). Kipaumbele cha pili muhimu ni ukuaji wa uchumi 16%, kulinda utambulisho wa Taifa (11%) na kulinda maliasili za Tanzania 11%, (Kielelezo cha 6).

[6] Kwa mujibu wa takwimu kutoka wizara ya fedha ya Tanzania na IMF/Benki ya Dunia, mwaka 2012 ruzuku za misaada zilifikia 29% ya mapato ya kodi za ndani (ruzuku 4.5% ya pato la taifa vs mapato ya kodi 15.8% ya pato la taifa; http:// ww.worldbank.org/tanzania/economicupdate, kiambatisho cha ki akwimu na 1).

**Kielelezo cha 6: Ni vipaumbele gani muhimu zaidi kwa siku zijazo?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 23 (Agosti 2014)

## Jambo la 6: Wananchi saba kati   a kumi wanaamini kuwa Tanzania itakuwa nchi yenye uchumi wa kati i    apo 2025

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Tanzania 2025 inalenga kuipeleka Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati i    apo mwaka 2025. Wananchi saba kati   a kumi wanaamini kuwa lengo hili litafiki   a (Kielelezo cha 7). Pamoja na hayo, karibu wananchi saba kati   a kumi (68%) wanatarajia kuona kuwa na Rais mwanamke kati  a miaka kumi ijayo. Kwa upande mwingine, Watanzania sita kati ya kumi wanatarajia kuendelea kwa migogoro ya kidini na kupotea kabisa kwa tembo (Kielelezo cha 7). Karibu nusu (51%) wanaamini kwamba Muungano utavunjika. Matukio yenye utabiri mdogo ni kama vile Tanzania kufuzu kushiriki Kombe la Dunia (38% wanaamini hili litatokea), na kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki chini ya Rais mmoja (33%) (Kielelezo cha 7). Wakati m  tarajio haya yalitofautiana kido  o miongoni mwa makundi mbalimbali ya watu, kundi la Wahitimu    a kidato cha nne lilielekea kuamini zaidi kuwa tembo watapotea kabisa, kwamba Tanzania haitafuzu kuingia Kombe la Dunia, na kwamba Muungano wa Tanzania utavunjika (takwimu hazijaoneshwa hapa).

Ikumbukwe kuwa takwimu hizi zilikusanywa mwezi Agosti 2014, na hazibebi mabadiliko ambayo yanayoweza kuwa yametokea kutokana na muelekeo wa kisiasa wa hivi karibuni.

**Kielelezo cha 7: Asilimia waliojibu “Ndiyo” katika uwezekano wa yafuatayo kutokea.**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Awamu ya 23 (Agosti 2014)

# 3. Hitimish

Kwa jumla tunayoweza kuona kutokana na takwimu hizi ni kuwa Watanzania wana matumaini makubwa juu ya nchi yao - hata kwa kuziangalia kimakundi kati ya wanawake na wanaume; mijini na vijijini, tajiri na maskini – lakini matumaini haya wakati fulani yanaonekana kukinzana na changamoto muhimu au matati o yanayowakabili wananchi.

Kwa mfano, Watanzania wawili kati a watatu wana matumaini makubwa kuhusu nchi yao, wanaamini kuwa ifi apo mwaka 2025 nchi itakuwa mahali pazuri pa kuishi (Jambo la 4). Hata hivyo, karibu wananchi wawili kati ya watatu wanabashiri kuwa kutatokea migogoro ya kidini ndani ya kipindi hicho hicho (Jambo la 7). Mitazamo hii inakinzana. Tafsiri mojawapo inaweza kuwa kwamba, wale wanaotarajia migogoro ya kidini, wanatarajia kuwa itakuwa migogoro midogo midogo tu, kwenye baadhi ya maeneo na kwa muda mfupi. Tafsiri nyingine inaweza kuwa kwamba, matarajio ya wananchi ya maendeleo chanya yana uzito mkubwa kuliko matarajio yao ya kuwepo kwa matukio hasi.

Hata hivyo, matarajio haya hayatofautiani mion oni mwa makundi ya wanaume au wanawake, wakazi wa mijini au vijijini, vijana au wazee. Tuligundua kuwa hakuna tofauti kubwa (kitakwimu) baina ya majibu yao na matarajio yao ya baadaye. Kwa mfano, vijana, wako sawa na wazee kati a kuamini kuwa Tanzania itakuwa sehemu nzuri ya kuishi ifi apo mwaka 2025.

Kuna njia mbalimbali za kutafsiri hoja hii ya kufanana kwa matarajio ya siku zijazo kati ya makundi mbalimbali ya wananchi. Kwanza, mtazamo uliozoeleka ni kuwa vijana wa Tanzania wana mitazamo tofauti na  atanzania wenzao wenye umri mkubwa, au kwamba kuna tofauti  ati  a wanaume na wanawake, au hata kati  a wakazi wa vijijini na wa mijini. Takwimu zimeonyesha kwamba mtazamo hii hauna ukweli. Ukweli ni kwamba makundi yote yanafanana kwa kiasi kikubwa kuhusu matumaini yao ya baadaye, na makundi yote yana wasiwasi unaofanana kuhusu migogoro ya kidini, nchi kugawanyika na pia kupotea kwa tembo. Je, kufanana huku kwa maoni kuhusu hali ya baadaye kwa makundi ya watu mbalimbali wa maeneo mbalimbali ya Tanzania kunatoa maelezo yoyote kuhusu utulivu wa kijamii uliopo nchini Tanzania? Hili ni wazo linalofaa kuchunguzwa zaidi.

Hivyo, baadae ya Tanzania itakuwaje? Kiuchumi, kuna hofu kuu mbili. Nchi inaweza kukabiliana na uhaba mkubwa wa fedha katika miaka ijayo, hii ikitokana na wafadhili wakubwa na wabia wa biashara huko Ulaya kukabiliwa na kuyumba kwa thamani ya Fedha ya Umoja wa Ulaya (Euro), matatizo ya uhamiaji, na kuendelea kuporomoka kwa uchumi kwa muda mrefu. Hii inaweza kuwa na athari hasi za muda mrefu kwenye kutoa misaada na kuchangia mapato kwa njia ya utalii nchini. Wakati huo huo, matarajio ya mapato makubwa kutoka kwenye gesi yanaweza yasitimie kama bei ya gesi kimataifa itaendelea kushuka kutokana na ongezeka kubwa la uuzaji gesi kimataifa linaloibuka kwa sababu ya kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi nchini Marekani, na pia kupungua kwa mahitaji ya gesi duniani[7](Jarida la Kiingereza). Uwezekano huu haukuchunguzwa katika utafiti wetu, lakini kuna uwezekano wa swala hili kuiathiri Tanzania katika kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kama inavyotarajiwa na Watanzania watatu kati ya wanne.

Matumaini ya pamoja ya Watanzania yanaweza kuwa kitu cha thamani miaka kati  a ijayo, hasa kwa sababu nchi inashughulika na mchakato wa kuwa na katiba m  ya, matarajio ya maliasili na utawala, ongezeko la ukuaji wa miji, kuyumba kwa uchumi wa dunia, na mapambano ya muda mrefu ya kupunguza umaskini. Changamoto, kwa Serikali ya Tanzania, wasomi wa ndani na wananchi wenyewe, ni kuhakikisha kuwa matumaini haya yanaendelezwa kupitia utun  aji sera na utekelezaji wenye ufanisi, kuhimiza maendeleo yenye usawa na kujenga mshikamano wa kijamii, ili matarajio ya wananchi ya maisha bora siku zijazo yaweze kufiki  a.

---

7 "East Africa May Lose Before It Even Enters Energy Game." Foreign Policy in Focus, October 15, 2014. http://  ww.foreign-policy.com/articles/2014/10/15 out_of_africa_mozambique_kenya_uganda_tanzania_oil_gas